

Ofisi ya Rais

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI
SHULE YA SEKONDARI PAUL MAKONDA**

S.L.P 366009,
DAR ES SALAAM,
TAREHE.....

Kumb.Na.PMSS/FK/1/2021

JINA LA MWANAFUNZI.....

S.L.P.....

DAR ES SALAAM.

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI
PAUL MAKONDA WILAYA YA KIGAMBONI
MWAKA 2021**

1.0 Nina furaha kujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na **KIDATO CHA KWANZA** katika Shule ya Sekondari Paul Makonda. Shule ipo kata ya Kigamboni karibu na Shule ya Msingi Ufukoni.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe.....Mwanafunzi akiwa na mzazi/mlezi wake anatakiwa kuripoti Shulenii tarehe.....kwa ajili ya usajili akiwa na vifaa vyote alivyoagizwa.(Siku ya kufungua Shule usajili hautafanyika).

2.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa siku ya kuripoti shulenii.

- i. Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla. Ni jambo la lazima
- ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
- iii. Kutimiza kwa makini kazi alizopewa shulenii.(home work)
- iv. Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

- v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- vi. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- vii. Kuvalaa sare za shule wakati wote unapokuwa kwenye mazingira ya shule kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

3.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, Ubakaji na Ushoga.
3. Ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevyta.
4. Uvutaji bangi.
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau bendera ya Taifa.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. a) Kijana wa kiume kuwa na nywele fupi, zilizo sawa kichwa kizima, wakati wote.
b) Kijana wa kike kuwa na nywele na fupi na kusuka nywele 5-7 wakati wote anapokuwa shulenii.
15. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki SIMU awapo shulenii ikikamatwa **HATARUDISHWA.**

16. Kuto kufanya mitihani bila sababu yoyote ya msingi.

17. Kuwa nje ya eneo la shule wakati wa masomo.

4.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATI

4.1 SARE ZA SHULE

- a) Sare ya shule ni suruali (2) rangi ya zabibu (Namba.1) na shati 2 nyeupe mikono mifupi kwa wavulana na sketi (2) ndefu rangi ya zabibu (Namba.1) na blauzi (2) mikono mifupi kwa wasichana na Wanaovaa Hijabu, Nusu kanzu mikono mirefu.
- b) Sare ya michezo kwa shule hii ni FULANA rangi ya kwa wavulana na kwa wasichana, itavaliwa siku ya Ijumaa tu.
- c) Rangi ya Hijabu ni Nyeupe ISIYO NA UREMBO na kubwa kufunika kiwiko cha mikono.
- d) Viatu vyeusi nya ngozi soli fupi, kwa wasichana na wavulana. Soksi ndefu nyeupe kwa wasichana na soksi fupi nyeusi kwa wavulana, sweta rangi yakwa wote.

4.2 MAHITAJI WAKATI WA USAJILI

1. Picha nne(4) za passport size za mwanafunzi na moja ya mzazi au mlezi wake akiwa amevaa sare ya shule.
2. Cheti cha kuzaliwa (kivuli).
3. Medical Examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali.Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shulenii.
4. Fomu ya maaelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
5. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na kiapo kwa mzazi.

6. Fomu zote ziwekwe kwenye faili (spring file) sio la plastiki.

7. MAHITAJI MENGINE MUHIMU

- i. Madaftari makubwa 9 (counter 3 quire)
- ii. Madaftari madogo (msomi 9).
- iii. Begi jeusi la kubebbea vifaa vya shule
- iv. Kalamu za kutosha za wino na penseli
- v. Rula ya sm 30 na kifutio.
- vi. Viatu vyeusi vya kutumbukiza
- vii. Soksi (nyeusi wavulana, nyeupe wasichana)
- viii. Mkanda mweuzi kwa wavulana
- ix. Kamusi mbili (dictionary) ya Kiswahili na English
- x. Mathematical set 1

4.3 VITABU VYA KUMNUNULIA MTOTO

Inashauriwa kumsaidia motto wako kumnunulia vitabu ambavyo vitakuwa mali yake kama orodha inavyoonesha hapo chini:

- i. KISWAHILI-Kiswahili Sekondari kidato cha 1 – TIE
- ii. ENGLISH-English for secondary school book 1-TIE
- iii. Hawa the Bus Driver & Mabala the farmer
- iv. HISTORY-History for secondary school book 1-TIE
- v. B/MATH-B/math for secondary school book 1-TIE
- vi. GEOGRAPHY-Geography for secondary school book 1-TIE & BY UJUZI
- vii. CIVICS-Civics for secondary school book 1-TIE
- viii. CHEMISTRY-Chemistry for secondary school book 1&2 -TIE
- ix. BIOLOGY-Biology for secondary school book 1 & 2-TIE
- x. PHYSICS-Physics for secondary school book 1-TIE

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo / maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA

.....
MOSHI H.MALILO

MKUU WA SHULE

0713 288023

Email:malilomoshi76@gmail.com



FOMU YA KUKUBALIWA KUJIUNGA NA AHADI

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI PAUL MAKONDA

S.L.P 36009,

DAR ES SALAAM.

KWA MWANAFUNZI

Mimi.....(jina kamili)

Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha.....Mwaka.....katika Shule ya Sekondari Paul Makonda.

NINAAHIDI KWAMBA

1. Nitatii Sheria zote za Shule kama nilivyozisoma
2. Nitaweka bidii katika masomo, kazi na shughuli zote kisheria
3. Nitashiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali, kuzalisha mali ilivyo bora bila kuitia hasara Shule kwa kuharibu au kupoteza malighafi (Raw Materials) ya kuzalisha mali.
4. Nitakuwa Mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali juu, mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wote hata nikiwa nje ya Shule kwa madhumuni ya kuipa na kutunza sifa ya Shule ya Sekondari Paul Makonda.

MUNGU NISайдIE

Saini ya Mwanafunzi.....

KWA MZAZI

Mimi(Jina la Mzazi/Mlezi).....

Mzazi /Mlezi wa.....

NINAAHIDI KWAMBA

1. Nitampatia mwanangu mahitaji ya Shule kama yalivyotajwa katika maelezo ya kijiunga na Shule

2. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote utakaohitajiwa (Maoni,adhabu) katika kumlea Mwanangu.
3. Nitamhimiza mwanangu kufanya mazoezi yake ya masomo nyumbani (home work) na kufatilia maendeleo yake na tabia yake kishule.
4. Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake.
5. Nitahakikisha Mwanangu hafiki na simu Shulenii wakati wote.

Saini.....JINA.....NAMBA YA SIMU.....

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI
SHULE YA SEKONDARI PAUL MAKONDA
FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI

1. Jina kamili la Mwanafunzi.....
2. Tarehe ya kuzaliwa.....
3. Taifa.....
4. Uraia.....
5. Dini.....
6. Shule aliyoysoma/alizosoma kabla ya kuja Shule ya Sekondari Paul Makonda.

SHULE YA MSINGI / SEKONDARI	TAREHE NA MWAKA ULIANZA	TAREHE NA MWAKA ULIOTOKA
i.		
ii.		
iii.		
iv.		

Saini ya Mwanafunzi:..... Tarehe:.....

B. MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la mzazi/mlezi.....
2. Utaifa;.....
3. Uraia:.....
4. Anuani ya Dar es salaam:.....
5. Sehemu anayoishi:.....
6. Mtaa:.....
7. Namba ya nyumba:.....
8. Namba ya simu:.....
9. Mjumbe Jina:.....

10. Mtendaji / Mwenyekiti wa Mtaa

JINA:.....Sahihi:.....

11. Eleza kama mtoto ana matatizo yoyote ya kiafya

.....

C: MAELEKEZO YA KIKAZI MZAZI /MLEZI

- i. Jina la mwajiri:.....
- ii. Anuani:.....
- iii. Kazi ya mzazi/mlezi:.....

KIAMBATANISHO C

**KIGAMBONI MUNICIPAL COUNCIL
PAUL MAKONDA SECONDARY SCHOOL**

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To be filled by Government Medical Officer and return to the HEAD OF SECONDARY SCHOOL P.O.BOX 36009 DAR ES SALAAM.

To the Medical

.....

.....

.....

A : Re

Please examine the above mentioned student and comment on his/her fitness by responding to the problems below Say YES or NO to each problem and If yes then STATE.

HEAD OF SCHOOL: Stamp DATE:.....

Insert (✓) in the boxes provided

- i. Hearing Yes [] or []
- ii. speech Yes [] or []

- iii. sight Yes () or ()
- iv. Physical Yes () or ()
- v. Deaf Yes () or ()
- vi. Short sight Yes () or ()
- vii. Any other.....
.....

B. Recommend if the student is fit for studentship (i) YES (ii) NO
.....
.....

C. Any other advice.....
.....

Name and Signature:..... Date:.....